KIJARIDA KUHUSU

# FIDIA KATIKA MASHAURI YA JINAI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

# FIDIA KATIKA MASHAURI YA JINAI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

SHUKRANI ........................................................................5
DIBAJI ........................................................................5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU........................................................................7
MAONO ........................................................................8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI ........................................8
LENGO KUU ........................................................................8
Utangulizi ........................................................................9
Fidia ni Nini ........................................................................10
Fidia katika mashauri ya jinai........................................10
Fidia kwa maumivu, hasara au kifo kutokana na kumsaidia polisi ........................................................12
Watu waliohukumiwa kutokana na kutambuliwa kimakosa kulipwa fidia ................................................13
Fidia katika kesi zisizo na msingi au usumbufu. ..............13
Fidia katika kesi za kujamiiana........................................15
Utaratibu wa kupata fidia ................................................15
Hitimisho........................................................................17

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani za dhati kwa mwanasheria wetu Wakili Richard Evance Manyota pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hususani ofisi ya Arusha kwa kukiandaa kijitabu hiki.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote

kuzifahamu. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika migogoro dhidi ya kisheria ambayo igeweza kuepukika kama mtu huyo angejua sheria husika. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufahamu au maelezo ya sheria husika. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia zaidi.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.**

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam. Pia Kituo kina ofisi nyingine Arusha na Dodoma.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## Utangulizi

Shauri la jinai huhusisha kesi inayomkabili mshtakiwa anayeshukiwa dhidi ya serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenda kosa ambalo hupelekea kifungo cha gerezani na au kupata adhabu nyingine kama vile kulipa faini, kufanya kazi za kijamii au kuwa chini ya uangalizi kwa kipindi fulani.
Lengo kuu la kijarida hiki ni kukuelimisha msomaji juu ya utaratibu wa kudai fidia katika mashauri ya jinai yaliyoanzia katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu Pamoja na namna ya kujipatia fidia yako kutoka katika amri iliyotolewa katika shauri la jinai.

Mara tu baada ya kupitia na kusoma kijarida hiki, msomaji atakuwa na uelewa mpana juu ya namna ya kudai fidia itokanayo na amri ya mahakama katika mashauri ya jinai katika Mahakama za Wilaya pamoja na Mahakama za Hakimu Mkazi.

## Fidia ni Nini

Fidia ni malipo anayopewa mtu mara baada ya kuathirika na kitendo cha jinai lililosababishwa makusudi au vinginevyo. Katika shauri lililopo mahakamani; fidia ni kifuta jasho au malipo anayopewa muathirika wa shauri fulani mara baada ya mahakama kujiridhisha pasi na shaka juu ya ujinai wa mshtakiwa husika.

## Fidia katika mashauri ya jinai

**Aina za fidia katika jinai.**

i. Malipo ya Fedha
ii. Kurudishiwa mali yako ikiwa katika hali nzuri
iii. Matibabu kwa gharama za mshtakiwa
iv. Fidia nyingine yoyote mahakama itakayoona inafaa.

Kwa kawaida, mashauri ya Jinai ni kesi dhidi ya Jamuhuri ya Serikali ya Muungano ambaye ndiye mlalamikaji dhidi ya mshtakiwa na au

mlalamikaji na mshtakiwa ambaye huhusishwa na utendaji wa kosa fulani lililoanishwa kuwa la jinai kwa mujibu wa sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 (marejeo ya mwaka 2019) pamoja na sheria nyingine mbalimbali zinazojinaisha baadhi ya vitendo.

Kwa mujibu wa sheria ya kanuni ya adhabu, mahakama za Tanzania pamoja na adhabu nyingine zina uwezo wa kutoa amri kwa muathirika kufidiwa sehemu ndogo ya kifuta jasho ili walau kupooza machungu yaliyo sababishwa na mhukumiwa katika shauri la jinai.

Zaidi, katika sheria ya kanuni ya adhabu, mahakama inapewa mamlaka zaidi kuwa mtu yeyote ambaye anapatikana na hatia ya kutenda kosa anaweza kuhukumiwa kulipa fidia kwa mtu yeyote aliyejeruhiwa na kosa lake na fidia hiyo inaweza kuwa ni nyongeza ya/au ni mbadala wa adhabu nyingine yoyote.
Vivyo hivyo, pale mahakama inapotoa adhabu

mbadala (mathalani; kuachiwa bila masharti na kuachiwa na masharti) ina uwezo wa kuamuru mhukumiwa husika kulipa fidia kwa mujibu wa sheria.

## Fidia kwa maumivu, hasara au kifo kutokana na kumsaidia polisi

Inawezekana usiwe umedhurika kwa kutendewa kosa wewe moja kwa moja kama ambavyo tumeona hapo awali, ila yamkini katika kusaidia jeshi la polisi kutekeleza majukumu yake ambayo pia ni wajibu wa kila raia kusaidia utekelezaji wa shughuli za jeshi la polisi pale inapobidi na/au inapohitajika, mtu anaweza kupata maumivu, hasara na au kifo.
Ni haki ya muathirika huyo kupata fidia kwa mujibu wa sheria na utaratibu utakaowekwa na sheria husika. Endapo muathirika husika wakati akisaidia jeshi la polisi atafariki, basi fidia husika italipwa au kupokelewa na wategemezi au wawakilishi wake halali kisheria.

## Watu waliohukumiwa kutokana na kutambuliwa kimakosa kulipwa fidia

Pale ambapo imethibitika katika ushahidi kwamba mtu ametiwa hatiani kwa kutambuliwa kimakosa na kusababisha kushitakiwa, kuadhibiwa au kupata hasara yoyote au maumivu, mtu huyo au mwakilishi wake kisheria kama mtu huyo atafariki, atakuwa na haki ya kupata fidia kama vile alikuwa muathirika wa makosa ya jinai.

## Fidia katika kesi zisizo na msingi au usumbufu.

Mahakama pia ina mamlaka ya kutoa fidia kwa mshtakiwa endapo itathibitisha pamoja na mambo mengine kuwa mashtaka dhidi yake yalifunguliwa pasi na kuwa na sababu za msingi. Iwapo katika kuachiliwa kwa mshtakiwa, mahakama ina maoni kwamba shitaka halikuwa na msingi, mahakama inaweza kuamuru mlalamikaji kumlipa mshtakiwa fidia

ya kiasi stahiki kwa usumbufu na matumizi ambayo aliyatumia kutokana na shtaka hilo, kama nyongeza katika gharama zake.

Pale mshtakiwa anapotiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote ambalo adhabu yake si kifo na inaonesha katika ushahidi kwamba mtu mwingine, ama/au siyo mwendesha mashtaka au shahidi katika shauri, amepata hasara ya mali au maumivu ya mwili kutokana na kosa lililotendeka na kwamba fidia ni ya msingi, kwa maoni ya mahakama, mtu huyo anaweza kufidiwa katika shauri la madai, mahakama inaweza, kwa ridhaa yake na kama nyongeza ya adhabu yoyote ile halali, kuamuru mtu aliyepatikana na hatia kumlipa mtu mwingine fidia hiyo, kwa mali au fedha kama mahakama itakavyoona haki na msingi.

## Fidia katika kesi za kujamiiana

Wakati mahakama inapomtia mtu hatiani kwa kosa la kujamiana, inaweza kutoa adhabu ya kulipa fidia ili kufidia hasara iliyosababishwa na mhukumiwa huyo. Malipo hayo yanaweza kupatikana kupitia shauri la madai atakalo lifungua mahakamani.

## Utaratibu wa kupata fidia

Endapo kuna ushahidi usiopingika kuwa mhukumiwa aliye amriwa kulipa fidia husika kwa muathirika ana mali inayofaa kuuzika kwaajili ya kulipa fidia kwa muathirika, mahakama inauwezo wa kutoa amri ya namna gani mali hiyo inaweza kuuzwa ili kuweza kulipia fidia husika.

Sheria inawezesha mtu yeyote anaye dai fidia kwa mujibu wa amri ya mahakama, kudai fidia hiyo husika kwa njia ya kufungua shauri la madai katika mahakama yenye mamlaka

ili kuweza kusikiliza shauri hilo na kutoa maamuzi ya namna fidia hiyo itakavyolipwa na au utekelezaji wa amri hiyo.

Zaidi, kwa mujibu wa sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai, aliyepewa fidia anaweza kupeleka maombi yake yakisindikizwa na kiapo katika mahakama ile ile iliyotoa maamuzi ya fidia ili kupata amri ya kutekeleza hukumu kwaajili ya utekelezaji wa amri ya kulipwa fidia iliyotolewa na mahakama ikiwemo kushikilia na/au kuuza mali ya mhukumiwa kwa ajili ya kutekeleza amri ya fidia iliyotolewa na mahakama.

**Kushindwa kulipa fidia**

Kwa mujibu wa sheria ya kanuni za adhabu, pale ambapo mahakama itatoa maamuzi ya kulipa fidia kwa muathirika na mhukumiwa akapuuza kutimiza amri hiyo, basi, mhukumiwa huyo anakuwa amedharau amri halali ya mahakama na hivyo mahakama ina uwezo wa kubadilisha

adhabu hiyo na kuwa kifungo cha gerezani kisichopungua miezi sita pamoja na faini ya kiwango cha shilingi za kitanzania elfu hamsini. Vivyo hivyo, katika adhabu zinazoweza kutolewa wakati mshtakiwa wa kosa la kubaka anapotiwa hatiani, mahakama ina weza kutoa amri ya kulipwa fidia kwa muathirika husika kama sehemu ya kuponya majeraha aliyopata wakati wa tukio husika.

## Hitimisho

Pamoja na mambo mengine mengi, ni muhimu kukumbuka kwamba fidia hutolewa pale tu ambapo umeumizwa na kitendo fulani na mahakama imetoa amri ya kulipwa na/au kupewa fidia ya kuumizwa huko. Ikumbukwe zaidi kuwa, mahakama imeweka utaratibu wa kudai fidia itokanayo na shauri la jinai na/au kusaidia jeshi la polisi katika kutekeleza majukumu yake au katika mashauri ya jinai yahusuyo kujamiiana umewekwa kwa mujibu

wa sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai pamoja na namna ya kufanya utekelezaji wa amri ya fidia kama kama ilivyoelezwa hapo awali.

Katika kitini hiki, ni matumaini ya Kituo kuwa umepata mwanga wa kutosha kuelewa utaratibu na namna ya kupata fidia itokanayo na kuhitimishwa kwa shauri la jinai. Zaidi, umeweza kufahamu namna ambavyo fidia huweza kutolewa katika mazingira mbalimali ikiwemo pale ambapo umeathirika au kuumizwa kutokana na kutoa msaada kwa jeshi la polisi wakati wa kusaidia jeshi hilo kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria.

Pia ni matumaini yetu kuwa umeweza kufahamu zaidi kuwa, utaratibu wa kupeleka maombi kwa kutumia kiapo na/au kufungua shauri la madai.

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

FORD FOUNDATION

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

Ministry for Foreign Affairs of Finland

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV